Yesu Kristo – Nabii, Kuhani, Na Mfalme

(Jesus Christ – Prophet, Priest, and King)

Na

Ellis P. Forsman

Yesu Kristo – Nabii, Kuhani, Na Mfalme

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Yesu Kristo – Nabii, Kuhani, Na Mfalme

Ebr. 1:1-4

Ebr. 1:1-4, "*Mungu ambaye zamani alisema na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi anasema na sisi katika Mwana,* **(Nabii)** *aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uwezo wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi* **(Kuhani)** *aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu* **(Mfalme)***; amefanyika bora kupita malaika kwa kadiri jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao.*"

Waraka kwa Waebrania unaweza kuitwa maelezo yenye uvuvio ya kitabu cha Walawi, kwa maana ndani yake mwandishi anaonyesha kwamba sherehe za ukuhani wa Kiharuni yamekua kikamilifu ndani ya Yesu Kristo, Kuhani Mkuu wa Wakristo.

Neno la msingi la mwandishi wa waraka huu ilikuwa ni kuwashawishi ndugu zake wa Kiebrania waliokuwa ndani ya Kristo kuwa wavumilivu hadi mwisho wa elimu yao ya Ukristo ambao ndiyo waliuanza, na wasirudi tena katika Uyahudi. Walikaribia kumuacha Kristo na wamfuate Musa.

Kulikuwa na sababu mbili katika hili:

- Wengi wa Wakristo hawa walitoka katika mazingira ya Kiyahudi, na tungeweza kutarajia kuteswa na viongozi wa Kiyahudi.
- Zaidi sana, hawa Wakristo wa Kiyahudi walijifunza chini ya kitengo cha Musa; tabia zao zote za kidini na mvuto wa kwanza ulitumika katika kuwaunga katika sherehe na mila za kiyahudi.

Kwa vile, walipotakiwa kufanya uchaguzi kati ya Yesu na Musa, suluhisho lao halikuwa tu linadhoofishwa na uoga wa kuteswa bali kwa upendo wao wa mila za kizamani na desturi.

Hawa Wakristo wa Kiyahudi walihitaji msaada na kutiwa moyo na ilimpendeza Mungu wao kutumiwa msaada huo kupitia Paulo, ambaye hapo awali alifikiria kufanya mambo mengi kinyume na jina la Yesu.

Mdo 26:9, "*Kweli mimi mwenyewe naliona ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingamana na jina lake Yesu Mnazareti.*"

Mtume Paulo anaanza waraka kwa kuonyesha ukuu wa Ukristo dhidi ya mfumo wa Musa, na anaendelea kufanya hivyo katika waraka wote.

Mtume aliyevuviwa anafanya kazi kubwa ya kumuwasilisha Yesu kama Nabii wao, Kuhani, Na Mfalme. Anafanya hivi pale anapotumia maneno matatu:

- "*Mungu anasema nasi katika Mwana.*" – Kristo ni Nabii.
- "*Akiisha kufanya utakaso wa dhambi.*" – Kristo ni Kuhani.
- "*Aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu.*" – Kristo ni Mfalme.

Kristo ni Kuhani

Maana ya "nabii": "kutoka katika Prophanai; 'pro' ikimaanisha 'kwa', na 'phanai', ikimaanisha 'kunena'; vile vile, 'kunena kwa'"; hivyo nabii ni yule anayenena kwa niaba ya mwingine.

Njia ambayo Mungu aliwasiliana mwenyewe na mapenzi Yake kwa wanadamu chini ya Agano la Kale:

"*Kwa sehemu nyingi.*"

Ufunuo wa Agano la Kale lilitolewa tu katika magombo. Musa, Daudi, Isaya na wengine walipokea tu kwa juu juu na nyaraka zilizokuwa na mapenzi ya Mungu ambayo hayakukamilika.

"*Kwa njia nyingi.*"

Mungu alikuwa na njia nyingi ya kuwasilisha mapenzi yake. Kwa wakati mmoja kwa kunena ana kwa ana, wakati fulani kwa maono.

Sauti ya Mungu ilimwijia Samweli alipokuwa analala; ikamwijia Eliya kwa upepo wa dhoruba amabo uliangusha milima na kuvunja mawe madogo madogo; kwa tetemeko la ardhi, kwa moto, na kwa sauti ndogo iliyosimama.

Lakini Mungu "*mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana.*"

"Aliyemweka kuwa mrithi wa yote."

Kama Mungu, Kristo alikuwa sawa na Baba. Fil. 2:6, "*Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho.*"

Lakini kama mpatanishi, alichaguliwa na Baba kuwa mrithi wa vitu vyote, ukuu wa Bwana wa mbingu na dunia.

"*Tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.*"

Kwa Yesu, Mungu aliufanya ulimwengu, vionekanavyo na visivyoonekana, mbingu na nchi.

- Yoh. 1:1-3, "*Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika.*"
- Kol. 1:16-17, "*Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi au usultani, au enzi au mamlaka, vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye.*"
- *Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake.*"
- Yuko katika binadamu, Mwana wa Mungu; na kama ndivyo, lazima ana asili iyo hiyo.
- Yoh. 1:14, "*Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.*"
- Kol. 1:15, "*Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.*"

Eikon – mfano, kiwakilishi, tabia, mfano halisi.

"Akivichukua vyote kwa amri ya uwezo wake."

Hiyo ni, kwa uwezo wa Neno lake lenye nguvu au agizo.

- Zab. 33:6, "*Kwa neno la BWANA mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.*"
- Zab. 33:9, "*Maana yeye alisema ikawa; nay eye aliamuru ikasimama.*"

Hivyo, Yesu aliamuru mawimbi na pepo kusimama na zilitii; aliongea na wenye pepo na zikatoka; alinena na waliokufa na wakafufuka.

Waamini mambo ya kisasa katika mfumo wake wanakataa tangazo hili la kwanza ya Kristo kuwa Kuhani wetu.

Waamini mambo ya kisasa wanamkubali Yesu kama mwalimu mkuu, mwanafilosofia mkubwa kama vile Pilato, Aristotle, na Socrates lakini hawasemi na Nikodemo:

Yoh. 3:2, "*Huyo alimwijia usiku akamwambia, Rabi twajua ya kuwa u mwalimu umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu*

awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye."

Kristo ni Kuhani

Ngazi ya ukuhani (chini ya sheria ya Musa) kiujumla ilikuwa tofauti na ile ya kuhani. Nabii alinena na watu kwa niaba ya Mungu, bali kuhani alinena na Mungu kwa niaba ya watu.

Vifungu viwili vya kwanza vya Waebrania vinaeleza katika uwasilishi wa mwandishi wa Yesu kuwa Kuhani mkuu; lakini vifungu vinane vinavyofuata vinamuwasilisha Kristo kama Kuhani Mkuu wa Wakristo.

Yeye ni, *"mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu."* Ebr. 3:1, "*Kwa hiyo ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu,*"

Ni Kuhani Mkuu anayefahamu mwanadamu na Mungu. Ebr. 4:14-16, "*Basi, iwapo tunaye Kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hakuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu na udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*"

Ni Kuhani Mkuu "*Kwa maana Melkizedeki huyo mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme akambariki; ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote (tafsiri ya jina lake kwanza ni mfalme wa haki, tena, mfalme wa Salemu, maana yake mfalme wa amani; hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu); huyo adumu kuhani milele. Basi angalieni jinsi mtu huyo alivyo mkuu, ambaye Ibrahimu baba yetu mkuu alimpa sehemu ya kumi ya nyara. Na katika wana wa Lawi nao, wale waupatao ukuhani, wana amri kutwaa sehemu ya kumi kwa watu wao, yaani ndugu zao kwa agizo la sheria, ijapokuwa wametoka katika viuno vya Ibrahimu. Bali yeye ambaye uzazi wake haukuhesabiwa kuwa umetoka kwa hao, alitwaa sehemu ya kumi kwa Ibrahimu akambariki yeye aliye na ahadi. Wala haikanushiki kabisa kwamba mdogo hubarikiwa na mkubwa. Na hapa wanadamu wapatikanao na kufa hutwaa sehemu ya kumi; bali huko yeye ashuhudiwaye kwamba yu hai. Tena yaweza kusemwa ya kuwa, kwa njia ya Ibrahimu hata Lawi apokeaye sehemu ya kumi alitoa sehemu ya kumi; kwa kuwa alikuwa katika viuno vya baba*

yake, hapo Melkizedeki alipokutana naye. Basi kama ukamilifu ulikuwapo kwa ukuhani wa Lawi; (maana watu wale waliipata sheria kwa huo); kulikuwa na haja gani tena ya kuhani mwingine ainuke; kwa mfano wa Melkizedeki wala asihesabiwe kwa mfano wa Haruni? Maana ukuhani ule ukibadilika hapana budi sheria nayo ibadilike. Maana yeye aliyenenwa hayo alikuwa mshirika wa kabila nyingine, ambayo hakuna mtu wa kabila hiyo aliyehudumia madhabahu. Maana ni dhahiri kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila ambayo Musa hakunena neno lo lote juu yake katika mambo ya ukuhani. Tena hayo tusemayo ni dhahiri sana zaidi, ikiwa ametokea kuhani mwingine mithili ya Melkizedeki; asiyekuwa kuhani kwa sheria ya amri iliyo ya jinsi ya mwili, bali kwa nguvu za uzima usio na ukomo; maana ameshuhudiwa kwamba, wewe u kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki."

Yeye ni Kuhani wetu Mkuu kutusaidia wakati wo wote wa hitaji. Ebr. 7:25, "*Naye kwa sababu hii aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee.*"

Yeye ni Kuhani Mkuu ambaye kupitia damu yake tunatakaswa na kuupata ukombozi wa milele. Ebr. 9:11-12, "*Lakini Kristo akiisha kuja aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayo kuwapo, kwa hema iliyokubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake isiyo ya ulimwengu huu, wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele.*"

Walimwengu wa kisasa katika mtazamo wake tofauti wanakataa udhihirisho huu wa pili kwamba Kristo ni Kuhani wetu. Wakisasa wanakataa kwamba Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu wa Wakristo.

Yupo tayari kumweka Yesu katika sehemu ya starehe pamoja na Buddha, Confucius, Muhamadi, na viongozi wengine wa dini za kidunia. Lakini onyesho linapofanywa kuwa Kristo ni kuhani wetu Mkuu kupitia mateso yake na kifo msallabani, wale wa kisasa wanaanza kupiga chafya.

1 Kor. 1:17, "*Maana Kristo hakunituma ili nibatize, bali niihubiri habari njema; wala si kwa hekima ya maneno, msalaba wa Kristo usije ukabatilika.*"

Kristo Mfalme

Hii inaweza kuwa ni wajibu wa nabii au kuhani.

Yesu alikaa lini katika mkono wa kuume wa Mungu? Kufuatia kufufuka kwake alipopaa kwenda mbinguni kukaa katika mkono wa kuume wa Mungu.

- Marko 16:19, "*Basi Bwana Yesu baada ya kusema nao alichukuliwa juu mbinguni akaketi mkono wa kuume wa Mungu.*"

- Efe. 1:19-23, "*Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia. Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*"

Yesu ataendelea kuwa na "*mamlaka yote … mbinguni na duniani,*" hata atakapokuja tena. 1 Kor. 15:24-26, "*Hapo ndipo mwisho atakapompa Mungu Baba ufalme wake, atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu. Maana sharti amiliki yeye hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti.*"

Wengine wanakataa udhihirisho huu wa tatu wa kifungu chetu; wanakataa kwamba Kristo hatawali sasa kama "*Mfalme wa wafalme.*"

Siku ya Pentekoste kanisa la Bwana lilipoanzishwa, mtume aliyevuviwa Petro akatangaza kwamba Mungu amemfufua Kristo "*kukaa katika kiti chake cha enzi.*" Mdo. 2:30, "*Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba kwa uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi;*"

Hivyo inafuatia kwamba kama hakai pale sasa, hajafufuliwa kutoka katika wafu; na kama hajafufuliwa katika wafu, kuhubiri kwetu ni bure.

1 Kor. 15:12-17, "*Basi ikiwa Kristo anahubiriwa ya kwamba amefufuka katika wafu, mbona baadhi yenu husema kwamba hakuna kiyama ya wafu? Lakini kama hakuna kiyama ya wafu, Kristo naye hakufufuka; tena kama Kristo hakufufuka basi kuhubiri kwetu ni bure na imani yetu ni bure. Naam, na sisi tumeonekana kuwa mashahidi wa uongo wa Mungu, kwa maana tulimshuhudia Mungu ya kwamba alimfufua Kristo, ambaye hakumfufua ikiwa wafu hawafufuliwi. Maana ikiwa wafu hawafufuliwi Kristo naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu.*"

Anatawala sasa katika mkono wa kuume wa Mungu, ataendelea kutawala hadi adui wa mwisho, mauti yataangamizwa.

- 1 kor. 15:24-26, "*Hapo ndipo mwisho atakapompa Mungu Baba ufalme wake, atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu. Maana sharti amiliki yeye hata awaweke maadui zake chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti.*"

- Ufu. 20:12-14, "*Nikawaona wafu wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Mauti na kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani hilo ziwa la moto.*"

Hitimisho

Hakika, Yesu Kristo ni Nabii, Kuhani, na Mfalme; lakini, vipi kama tukimkataa?

Kama hatutamsikiliza Nabii, basi "*twende kwa nani?*" Yohana 6:68, "*Simoni Petro akajibu akisema, Bwana twende kwa nani? Wewe una maneno ya uzima.*"

Kama hatutakubali dhabihu ya Kuhani Mkuu huyu, tutatakaswa wapi dhambi zetu? Ebr. 10:26, "*Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi.*

Kama tukikataa mamlaka ya Mfalme wa wafalme, ni nani atatusaidia wakati wetu wa kufa?

- Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia mimi ndimi njia kweli na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"

- Ebr. 2:3, "*Sisi je tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitishwa kwetu na wale waliosikia.*"

  Hakuna kutoroka; hakuna njia nyingine ya wokovu, na wanaokataa ujumbe huu watafuatwa na maangamizi fulani.